# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA THELATHINI NA SABA

**26 MEI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________

## MKUTANO WA TATU

### KIKAO CHA THELATHINI NA SABA – TAREHE 26 MEI, 2026

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa

Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**436. MHESHIMIWA OTHMAN MAULID SULEIMAN (MAHONDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni ipo haja ya kutoa Stika za maegesho ya mwaka mzima kwa vyombo vya moto ili kupunguza usumbufu na kuongeza mapato.

**437. MHESHIMIWA DKT. SELEMANI SAIDI JAFO (KISARAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Mamlaka ya Mji Mdogo Kisarawe itapandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji na eneo la Vijijini kuwa Halmashauri mpya ya Wilaya Maneromango.

**438. MHESHIMIWA EMMANUEL JOHN KHAMBAY (BABATI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itanunua Gari la Taka kwa ajili ya Halmashauri ya Mji Babati.

**439. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Wodi ya upasuaji ya Wanawake na Jengo la kuhifadhia Maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Karatu.

**WIZARA YA UJENZI:**

**440. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Mwabomba – Ubagwe hadi Ulowa Kasenga inayounganisha Mikoa mitatu.

**441. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaweka Taa za Barabarani katika Miji ya Ilunga, Lugeye, Kabila, Kahangara, Hayabuyaga, Ng’haya na Mahaha.

**WIZARA YA KILIMO:**

**442. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka Sera mahususi ya kuongeza tija kwenye Sekta ya Kilimo kwa Mikoa ya Kanda ya Kati.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**443. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kujenga Viwanda vya Parachichi katika Jimbo la Lupembe.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**444. MHESHIMIWA ESTER AMOS BULAYA (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Vijana wa Bunda watanufaika na Mradi wa Ufugaji Samaki wa Vizimba kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

## WIZARA YA MADINI:

**445. MHESHIMIWA BARAKA ULIMBOKA MWAMENGO (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Serikali itawalipa waliokuwa Watumishi katika Mgodi wa Kiwira.

**446. MHESHIMIWA FAGASON ARON NKINGWA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Serikali itatenga maeneo ya Wachimbaji Wadogo na kuwapatia leseni za uchimbaji.

## WIZARA YA MAJI:

### 447. MHESHIMIWA ENOCK ZADOCK KOOLA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha ukarabati na uboreshaji wa Skimu ya Maji Marangu.

### 448. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakarabati na kupanua vyanzo vya Maji katika Kata za Lukozi, Malindi na Manolo ili viendane na mahitaji ya sasa.

## WIZARA YA AFYA:

### 449. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha huduma ya Afya kwa akina Mama Wajawazito na Watoto.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **26 MEI, 2026** | **KATIBU WA BUNGE** |